JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

S. L.P 1055, ARUSHA
Simu : (027) 2503538/ 2507928
Nukushi: (027) 2505973
Barua pepe: rbcarusha@pccb.go.tz
Wavuti : www.pccb.go.tz

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

JULAI 30, 2020

TAKUKURU ARUSHA YAOKOA SHILINGI MILIONI 195.6 ZA WAJASIRIAMALI WALIOKUWA WAMEDHULUMIWA

Katika tukio la kwanza:

Kwa kipindi cha mwezi Julai, 2020 TAKUKURU Mkoani Arusha imeokoa fedha jumla ya shilingi milioni mia moja tisini, laki moja sitini na tatu, mia nane hamsini (Shilingi 190,163,850/). Kiasi hiki cha fedha kilichookolewa ni sehemu ya jumla ya shilingi milioni mia mbili themanini na tisa, laki mbili sitini na moja,mia tatu na tatu (Shilingi 289,261,303/-) za wajasiriamali sita wa Jijini Arusha walizokuwa wamedhulumiwa na wamiliki wa Kiwanda cha Kijenge Animal Products Limited cha Jijini Arusha.

Ili kuhakikisha kwamba fedha hizi ambazo zilikuwa ni za mauzo ya mazao ya Wajasiriamali hao yaliyopokelewa na kiwanda hicho tangu Januari 2020, TAKUKURU Arusha inaendelea na uchunguzi huu na kiasi kilichosalia shilingi 99,097,453/- zinalipwa na watuhumiwa ndani ya mwezi mmoja. Fedha zilizookolewa zipo katika mchanganuo ufuatao:

1. Michael Mtana -Tsh 50,725,450/-
2. Issa Mush -Tsh 53,258,000/-
3. Keneth Lauwo - Tsh 19,639,200/-

4. Gregory Mukabi -Tsh 24,125,760/-
5. Leo Marandu -Tsh 28,793,040/-
6. Ahmed Mavura -Tsh 13,622,400/-

Katika tukio la pili,

Ofisi ya TAKUKURU mkoani Arusha imefanikiwa kumrejeshea mfanyabiashara Advera Kyaruzi fedha kiasi cha shilingi milioni tano, laki nne na themanini elfu (**Shilingi 5,480,000/-)** ambacho ni sehemu ya jumla ya shilingi milioni kumi na tano (shilingi 15,000,000/-) alichokuwa amedhulumiwa na wafanyabiashara wenzake GERVAS ANDREA MOLLEL na JOSEPH CHRISTOPHER MOLLEL tangu mwaka 2018.

Ili kuhakikisha kwamba fedha hizi ambazo zilikuwa ni za mzigo wa biashara uliotapeliwa na Gervas Mollel na wenzake, TAKUKURU Mkoani Arusha inaendelea na uchunguzi huu kuhakikisha fedha zilizobaki zinalipwa na watuhumiwa.

Ufafanuzi wa Makosa:

Katika tukio la kwanza:

TAKUKURU Mkoani Arusha, ilipokea taarifa mnamo tarehe 08.07.2020 kutoka kwa wajasiriamali sita wa Jijini Arusha ambao ni Albert Nicolaus Macha, Michael Donald Mtana, Leu Marandu,Gregory Mkabi, Keneth F. Lauwo na Ahmed Mavura wakieleza kwamba waliuza mazao (NAFAKA) kwa kampuni ya Kijenge Animal Products iliyopo Arusha kwa nyakati tofauti tangu mwezi Januari 2020 lakini hadi sasa hawajalipwa fedha zao jumla ya Shilingi milioni mia mbili themanini na tisa, laki mbili sitini na moja,mia tatu na tatu (**Shilingi 289,261,303/-**).

Wajasiriamali hao walieleza kwamba baada ya kudai kwa muda mrefu bila mafanikio waliamua kupeleka lalamiko lao kwa Mkuu wa Wilaya ya Arusha mnamo tarehe 28.05.2020. Mkuu wa wilaya aliwaita wamiliki wa kampuni hiyo ili kujibu tuhuma na wakamtuma Mwanasheria wa Kampuni kwa jina la Mike Honest ili awawakilishe. Katika mazungumzo yao na Mkuu wa Wilaya, Mwanasheria huyo aliahidi kwa maandishi kuwa kampuni itawalipa wafanyabiashara hao ifikapo tarehe 01.07.2020.

Hata hivyo, Ilipofika tarehe hiyo, watuhumiwa hawakulipa fedha hizo na wala hawakufika ofisi ya Mkuu wa Wilaya kutoa mrejesho. Kutokana na sababu hiyo, Mkuu wa Wilaya aliwaandikia barua ya wito watuhumiwa kwa mara nyingine lakini bado hawakufika na badala yake waliandika barua ya kueleza kuwa, wadai hao wawe wavumilivu vinginevyo waangalie mahali sahihi pa kupata haki yao badala ya kusumbua ofisi za Serikali na ndipo TAKUKURU Mkoa wa Arusha ilipoingilia kati na kufanikisha urejeshaji huu wa fedha.

Katika tukio la pili:

TAKUKURU Mkoani Arusha ilipokea taarifa kutoka kwa mfanyabiashara Advera Kyaruzi mkazi wa Mto wa Mbu wilayani Monduli akiwalalamikia wafanyabiashara wenzake GERVAS ANDREA MOLLEL na JOSEPH CHRISTOPHER MOLLEL - wote wa Kata ya OLTRUMET wilayani Arumeru kwa kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu kiasi cha shilingi milioni kumi na tano (sh.15,000,000/-).

Awali ilielezwa kwamba wafanyabiasha hao wote walikuwa wakishirkiana katika kusafirisha mbegu za vitunguu kutoka Tanzania kwenda Uganda lakini mnamo MWEZI Septemba, 2018 baada ya kupakia mzigo ukiwemo wa Advera wenye thamani ya sh 15,000,000/- walikubaliana kuwa, Advera Kyaruzi , Gervas Andrea na Haruna Kitundu watangulie kwa basi kwenda mpaka wa Murongo ambako wangekutana na Joseph Christopher ambaye alikuwa dereva wa FUSO yenye namba T 449 ATT iliyokuwa imebeba mzigo huo wa mbegu za vitunguu.

Safari ilikuwa hivyo kama walivyokuwa wamepanga lakini walivyofika Mpakani, Gervas alimtambulisha Advera kijana mwingine wa kuvuka naye mpakani. Baada ya hapo, kila Advera alipojaribu kuwasiliana na Christopher (Dereva wa fuso) kwa simu hakupatikana na hakuweza kumuona tena wala kupata mzigo wake. Tangu kipindi hicho Advera amekuwa akifuatilia fedha zake kutoka kwa watuhumiwa bila mafanikio.

TAKUKURU Mkoa wa Arusha inawashukuru wananchi wa mkoa wa Arusha kwa ushirikiano wanaoutoa kwa taasisi kwa kutoa taarifa za wanaojihusisha na vitendo vya rushwa kwenye taasisi za Serikali na maeneo mengine na kuwataka kuendelea na moyo huo.

TAKUKURU mkoa wa Arusha inawahakikishia kuendelea kufanyia kazi kwa uharaka taarifa zote zinazopokelewa ili kuwezesha haki kupatikana kwa wakati. Pia inawaasa wafanyabiashara na wawekezezaji kuwa waaminifu, na kuendesha shughuli zao kwa kufuata sheria, kanuni na taratibu.

Aidha inawaonya kuacha kuwadhulumu wale wote wanaoshirikiana nao katika shughuli zao hasa za biashara, kwani watakapobainika kufanya hivyo, TAKUKURU haitasita kuwakamata na kuwachukulia hatua kali za kisheria.

Kupambana na Rushwa ni jukumu langu.

Imetolewa na:

Signed

James G. Ruge – 0738 150 063
KAIMU MKUU WA TAKUKURU (M) ARUSHA